# KUWEKA WAZI HALI YA MAAMBUKIZI YA VVU NA UPIMAJI WA WENZA AU MWENZI NA WATOTO WA MVIU WALIO NA UMRI CHINI YA MIAKA 15

A

1. Kuweka wazi hali ya maambukizi ya VVU ni nini?
2. Je, ni rahisi kwa MVIU kuweka wazi hali yake ya maambukizi ya VVU kwa rafiki yake au familia? Kwanini Ndiyo au Hapana?
3. Kuna manufaa gani kwa MVIU kuweka wazi hali yake ya maambuki ya VVU?
4. Namna gani MVIU anaweza kusaidiwa kuweka wazi hali yake ya maambukizi ya VVU kwa rafiki wa karibu au familia?
5. Upimaji wa VVU kwa wenza na watoto wa MVIU ni nini?
6. Kuna umuhimu au faida gani kwa MVIU kuhakikisha mwenza/wenza wake na watoto wake wanapimwa VVU?



Furaha Yangu!

## UJUMBE MUHIMU:

- Ni muhimu kuweka wazi hali ya maambukizi ya VVU kwa watu wako wa karibu kama rafiki au mwanafamilia unayemuamini ili kuimarisha na kuboresha ufanisi wa matibabu, kinga na matunzo. WAVIU wote wahamasishwe kuweka wazi hali zao za maambukizi ya VVU kwa wenza au mwenzi, wanafamilia, marafiki wa karibu wanao waamini na jamii ili waweze kutoa usaidizi kwa MVIU. Hii itamuwezesha na kumrahisishia MVIU kupata huduma rafiki na endelevu za matibabu ya VVU ikiwa ni pamoja na kukumbushwa kunywa dawa kila siku na kwa wakati aliojipangia, kuhudhuria kliniki na kutimiza miadi ya matibabu ili aweze kufanikiwa kufubaza au kupunguza kiwango cha VVU mwilini na hivyo kupunguza uwezekano wa kuambukiza VVU wengine kwa njia ya ngono, na kwa wanawake wajawazito na wanao nyonyesha kupunguza uwezekano wa kuwaambukiza watoto wao VVU.

- Huduma ya upimaji wa VVU kwa wenza na watoto wa MVIU ni huduma ya ufuatiliaji wa wenza (mwenzi) wa kingono na Watoto wa MVIU (waliochini ya umri wa miaka 15) ili kuwapima VVU. Mara MVIU anapogundulika kuwa anamaambukizi ya VVU hushauriwa kutaja mtandao wake wa kingono (watu alioshiriki nao ngono ndani ya kipindi cha miezi 12) pamoja na Watoto ili wapate huduma ya upimaji VVU kwa hiari.

- Huduma hii hutolewa ili kuwawezesha WAVIU wote kujua hali zao za maambukizi ya VVU, na kufahamu jinsi ya kuhakikisha wenzi na Watoto wao wanataarifiwa kuhusu hatari ya kuambukizwa VVU. Pia huduma hii inasaidia kumuunganisha MVIU, wenza au mwenzi wake na watoto kwenye huduma za tiba, kinga na matunzo ili kuimarisha afya zao na kupunguza hatari ya kuambukiza au kuambukizwa VVU.